



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA



03/01/2025

TANGAZO LA KAZI YA MKATABA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Tunduma anawatangazia wananchi wote wenye sifa zilizoainishwa kwenye tangazo hili kuomba nafasi za kazi ya mkataba wa miezi mitatu (03) ya ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri.

WAKUSANYA USHURU (MAKARANI) - NAFASI 90

KAZI NA MAJIKUMU.

1. Kukusanya Mapato ya ndani ya Halmashauri kwa kutumia Mashine za Kielectronic za kukusanya Mapato (POS)
2. Kuhakikisha Fedha inayokusanywa inapelekwa Bank katika akaunti za Halmashauri kwa wakati
3. Kuhakikisha Mapato yote yanayopaswa kukusanywa na Halmashauri yanakusanywa kwa usahihi
4. Kutunza kumbukumbu za Hesabu
5. Kutunza vizuri mashine za kukusanya Mapato (POS)
6. Kutoa na kuwasilisha taarifa za makusanyo ya kila siku kwa Halmashauri
7. Kufanya kazi nyingine atakazo pangwa na Msimamizi wake

NB: MSHAHARA KWA MWEZI SHILINGI 200,000 (LAKI MBILI KWA MWEZI)

Kuajiriwa wenye Elimu ya kuanzia Astashahada (Certificate) na kuendelea ambao wana uelewa wa kutumia simu janja (Smart phone), sababu Mapato yote ya Serikali yanakusanywa kwa kutumia Mashine za Kielectronic za Kukusanya Mapato (POS) ambayo ina application sawa na simu janja. Aidha waombaji wenye sifa Zaidi ya zilizotajwa hapo juu maombi yao hayatafikiriwa

MASHARTI YA WAOMBALI KATIKA KAZI HII

1. Awe ni raia wa Tanzania
2. Awe amehitimu kidato cha Nne /sita
3. Asiwe Mwajiriwa wa Serikali
4. Awe na Umri wa kati ya 18 - 45
5. Muadilifu asiye na Kasoro yoyote
6. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheieza (Detailed CV) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina mawili ya Wadhamini Watumishi wa Umma (Referees) na anwani zao sahihi na namba za simu.
7. Maombi yaambontane pamoja na nakala ya vyeti vyote vya kitaaluma, na Cheti cha kuzaliwa vya Mwombaji.
8. Awe na Kitambulisho cha Taifa / Namba ya NIDA
9. Awe tayari kupangiwa kituo chochote cha kukusanya Mapato ndani ya Mji wa Tunduma.
10. Awe Muaminifu katika kukusanya Mapato ya Serikali na kuhakikisha fedha ya Serikali haipotei.
11. Awe tayari kutii na kufuata maelekezo atakayopangiwa bila kuvunja misingi ya Sheria ndogo ving'go za Halmashauri.

JINSI YA KUTUMA MAOMBI:

Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na anwani kamili ya Mwombaji pamoja na namba ya simu na zitumwe kwa anuani ifuatayo;


MKURUGENZI WA MJI,

S.L.P 73,

TUNDUMA.

TAREHE YA MWISHO YA KUPOKEA MAOMBI:

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 17/01/2025 saa 9:30 Alasiri


Mariam Chaurembo
MKURUGENZI WA MJI

MKURUGENZI WA MJI
HALMASHAURI YA MJI
TUNDUMA